

## **HOTUBA YA MKURUGENZI MKUU WA SHIRIKA LA RELI TANZANIA- TRC NDG. MASANJA KUNGU KADOGOSA KATIKA HAFLA YA UZINDUZI WA MFUMO WA TIKETI ZA KIELEKTRONIKI (e-TICKETING SYSTEM) LINALOFANYIKA TAREHE 4.4.2020**

Mh. Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mh. Mhandisi Isack Kamwelwe,

Mh. Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi ya shirika la Reli Tanzania Prof. John Kondoro,

Mtendaji Mkuu wa mamlaka ya Selikali mtandao (eGa),

- Menejimenti ya shirika la reli Tanzania
- Wafanyakazi wa TRC
- Wageni waalikwa na
- Wanahabari

Habari za asubuhi Mabibi na Mabwana

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha kukutana leo hapa kwa dhumuni la kushuhudia hafla ya uzinduzi wa mfumo wa tiketi wa kielektroniki wa shirika la Reli Tanzania.

Pia napenda kutoa shukurani zangu kwa Mheshimiwa Waziri Ujenzi, Uchukuzo na Mawasiliano kwanza kwa kukubali mwaliko wa TRC kuwa mgeni rasmi katika tukio hili lakini pia kwa kuendelea kuongoza dhamira ya dhati ya Serikali kuliwezesha Shirika la reli-TRC lirudishie uwezo wa ufanisi kwa hatua za kuimarisha uendeshaji wake na miundombinu ya reli ili iweze kujiendesha kiushindani ndani ya nchi na kikanda.

### **Ndugu Mgeni Rasmi**

Tutakuwa wakosefu wa fadhila endapo hatutatoa shukurani zetu za dhati kwa Serikali ya awamu ya tano chini ya Mheshimiwa Rais Dr. John Pombe Magufuli, kwani tangu ilipoingia madarakani 2015, ilitoa kipaumbale cha kuendeleza sekta ya reli ikiwa pamoja na dhamira ya dhati ya kurejesha usafiri wa reli kuwa wa uhakika na salama.

### **Ndugu Mgeni Rasmi**

Shughuli za kibiashara za Shirika la Reli Tanzania zimegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo :

- i. Huduma za Usafishaji wa Abiria wa kwenda mikoani kuelekea kanda ya kati, Kigoma, Mwanza na Mpanda na Kanda ya Kaskazini kuelekea Moshi na Arusha.
- ii. Huduma za Usafishaji wa Mizigo
- iii. Huduma za usafirishaji abiria katika jiji la Dar es Salaam (Commuter train) kati ya stesheni kwenda Pugu na Ubungo.
- iv. Huduma zinginezo ambazo si za usafirishaji kama vile za ukodishaji wa nyumba, na viwanja (real estate) na ukodishaji wa mitambo.

Katika kuimarisha na kuboresha huduma zake za usafiri wa abiria na mizigo pamoja na utekelezaji wa maelekezo ya serikali yanayotaka taasisi zote za umma zinazojihusisha na ukusanyaji wa mapato zifanye hivyo kwa njia za kielektroniki, Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) wametengeneza mfumo wa Tiketi wa kielektroniki (e-Ticket) na Malipo ya mizigo kwa Njia ya Mtandao (e-Cargo).

### **Historia ya Mfumo**

**Ndugu Mgeni Rasmi**, kazi ya utengenezaji wa mfumo wa tiketi wa kielektroniki ulianza mnamo tarehe Juni , 2018 na kuanza kutumika kwa majaribio mnamo mwezi wa Desemba 2018 kwa kutumika katika stesheni zote kubwa za reli ya kati na baadae kusambazwa kwenye stesheni ndogo kwenye reli hiyo.

Mwezi wa Kumi na mbili mwaka 2019 mfumo huu pia ulisambazwa na kuanza kutumika kwenye reli ya kaskazini kuelekea Moshi wakati reli hiyo inafunguliwa kuanza kutumika tena kwa usafirishaji wa abiria. Mpaka sasa mfumo unatumika katika jumla ya vituo 71 vya reli kukatia tiketi na kupokelea mizigo nchi nzima.

Kazi zote kutengeneza mfumo huu zimefanywa na wataalamu wa ki-tanzania wafanyakazi wa eGA na Shirika la reli Tanzania-TRC.

Pia mafunzo mbalimbali yameendeshwa kwa watumiaji mbalimbali wa mfumo huu wakiwemo wakatishaji tiketi, wasimamizi wa Stesheni, wakaguzi wa tiketi pamoja na makarani wa kitengo cha usafirishaji mizigo na hivyo kuwapatia uwezo wa kutumia mfumo huu ipasavyo.

### **Ndugu mgeni rasmi**

Mfumo huu wa tiketi wa kielektroniki umeunganishwa na mfumo wa malipo ya Serikali yaani *Government electronic Payment Gateway (GePG)* na ni mkusanyiko wa mifumo midogo minne ambayo ni:

- i. Mfumo wa ukataji wa Tiketi kwa njia ya Mtandao (e-Ticketing system)
- ii. Mfumo wa usimiamizi wa biashara ya mizigo kwa njia Mtandao (e- Cargo System)
- iii. Mfumo wa ukataji tiketi za abiria wa treni za mijini (commuter train) katika jiji la Dar es Salaam.
- iv. Mfumo wa ukusanyaji wa malipo ya huduma nyinginezo (Other services) zitolewazo na shirika kwa mfano malipo ya pango za nyumba na ardhi

### **1. Mfumo wa tiketi za abiria kielektroniki (e-Ticketing system)**

**Ndugu Mgeni Rasmi**, mfumo wa ukataji tiketi za abiria kwa safari za treni za mikoani ni mfumo unaotumika katika ukatishaji tiketi katika vituo na stesheni za reli. Mfumo huu pia unawawezesha abiria kukata na kulipia tiketi wao wenyewe kwa njia ya mtandao bila kuhitajika wao kwenda kwenye vituo vya kukatia tiketi. Mfumo hutumika pia kuwapatia abiria taarifa mbalimbali kuhusu mabadiliko ya ratiba kwa kutumia ujumbe mfupi wa SMS.

### **2. Mfumo wa usimamizi wa biashara ya mizigo (e-Cargo)**

**Ndugu Mgeni Rasmi** sehemu nyingine ya mfumo wa tiketi wa kielektroniki ni ule unaotumika kuratibu biashara ya Mizigo kwa njia ya Mtandao. Mfumo huu umewawezesha wateja wa usafirishaji wa mizigo kulipia gharama ya usafirishaji wa mizigo yao kwa njia ya mtandao baada ya kupewa gharama hizo na maofisa wa shirika bila kuhitaji kurudi kwenye ofisi za shirika kwa ajili ya kufanya malipo hivyo kuondoa upokeaji wa fedha taslimu.

### **3. Mfumo wa kukusanya mapato ya huduma nyinginezo zitolewazo na shirika (Managed bill)**

**Ndugu Mgeni Rasmi**, Mfumo pia una moduli inayowezesha shirika kutoa ankara kielektroniki kwa wateja wa huduma nyingine ambazo si zile za msingi za shirika la Reli. Wateja wanapewa ankara zao zenye namba ya malipo (*control number*) na hivyo kuweza kulipa kupitia njia mbalimbali za malipo na hivyo kuzuia upokeaji wa fedha taslim.

#### **4. Mfumo wa ukataji tiketi wa abiria wa treni za mijini (commuter train)**

**Ndugu Mgeni Rasmi**, Mwisho mfumo una moduli ya ukataji tiketi za abiria wa treni za mijini -jijini Dar es salaam- inayoweza ukataji wa tiketi kwa njia ya kielektroniki. Mfumo huu unaondoa utaratibu wa ukataji tiketi kwa kutumia vitabu na umekamilika kutengenezwa mwishoni mwa mwezi wa tatu mwaka huu 2020 na kwa sasa uko katika majaribio.

#### **Faida za Matumizi ya Mfumo**

Tangu kuanza kutumika kwa mfumo huu kumekuwa na faida kadhaa zikiwemo:

1. Tangu mfumo uanze kutumika mwezi Dec,2018 jumla ya sh 42.39 bilioni zimekusanywa kupitia mfumo huu. Hii ikiwa ni pamoja na tiketi za abiria zipatazo 425,016.
2. Kumekuwa na ongezeko la ukusanyaji wa mapato ukilinganisha na kipindi ambacho mfumo ulikuwa hautumiki kutoka wastani wa sh 3.066 billioni kwa mwezi hadi wastani wa sh 3.4 billioni
3. Kuwapunguzia abiria usumbufu wa kuja stesheni ili waweze kupata tiketi za safari.
4. Mfumo umepunguza gharama za mbalimbali za uendeshaji kwa mfano gharama za uchapishaji wa vitabu vya tiketi, usimamizi wa hela taslimu na kurahisisha ufuatiliaji wa shughuli za kiasibu.
5. Umerahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali zinazohusiana na usafirishaji wa abiria na mizigo na hivyo kuwezesha shirika kupanga mipango yake kwa uweledi Zaidi
6. Mfumo kutengenezwa kwa kutumia wataalamu wazawa walio katika taasisi za serikali yaani eGa na TRC kumeokoa fedha nyingi na uzoefu uliopatikana kwa kutengeneza mfumo huu unaweza kutumika katika sekta na mashirika mengine ya usafirishaji ya umma kwa gharama nafuu

#### **Ndugu Mgeni Rasmi ,**

Pamoja na mafanikio ya Mfumo huu wa Tiketi , Shirika la reli linaendelea na juhudi zake za kuendelea kuboresha huduma zake na uendeshaji kutumia teknolojia ili kupunguza gharama na kuongeza ufanisi katika shughuli zake zote. Kwa mfano kwa wakati huu kwa kushirikiana na eGA shirika linatekeleza miradi mbalimbali

ikiwamo wa mradi wa ofisi mtandao (e-office) na mfumo wa usimamizi wa rasilimali za shirika (Enterprise Resource management systems- ERMS) pamoja na kufufua na kukarabati miundombinu ya mtandao katika ofisi za shirika.

Mwisho kabisa naomba nichukue nafasi kuwashukuru mamlaka ya serikali mtandao eGA kwa ushirikiano wao mkubwa ambao wameuonyesha katika kuujenga na kuuendeleza mfumo huu. Ushirikiano wetu umeonyesha kuwa kumbe pamoja tukiamua tunaweza kufanya mambo makubwa sana. Tunaomba ushirikiano huu uendelee ili tulete tija zaidi kwa shirika na taifa kwa ujumla.

Asanteni sana.

**RELI YETU, MAENDELEO YETU, TAIFA LETU**